**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**
JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI

# KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA

## MTAALA WA SHULE ZA MSINGI

## GREDI YA 3

Chapisho la Kwanza 2017

Chapisho la Pili 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN: 978-9914-43-071-4
Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

**DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU**

Serikali ya Kenya imejitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera ya elimu, mafunzo na utafiti yanatimiza maazimio ya Katiba ya Kenya, 2010, Ruwaza ya Kenya, 2030, Sera ya Mtaala ya Kitaifa ya 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na mikataba ya kieneo na kimataifa ambayo Kenya ni mshirika. Katika kutimiza kauli mbiu ya Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu imefanikiwa kuanzisha utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika viwango vya Chekechea, Shule za Msingi na Shule za Junia.

Utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi unahusisha ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kwamba umefanikiwa. Baada ya kutekelezwa kwa mtaala huu kwa awamu ya kwanza ya miaka mitano, tathmini tamati ya utekelezwaji huu ilifanywa ili kubaini iwapo matokeo yanayotarajiwa kama yanavyoelezewa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) yalifikiwa. Serikali ya Kenya iliunda jopokazi ya Rais ya: *Presidential Working Party on Education Reforms* (PWPER) mwaka wa 2022 kushughulikia masuala nyeti yanayotatiza sekta ya elimu. Jopokazi hii ya rais ilitoa mapendekezo mbalimbali yanayoathiri elimu nchini yaliyochochea kutazamwa upya kwa mtaala wa elimu. Mapendekezo ya jopokazi hii, ripoti za kuangalia utekelezaji wa mtaala, ripoti za tathmini tamati kuhusu utekelezwaji wa elimu ya msingi kiawamu na taarifa kutoka kwa wanaotekeleza mtaala na washikadau wengine zilichangia usawasishaji na kutazamwa upya kwa mtaala wa elimu ya awali. Mtaala uliofanyiwa marekebisho wa shule za msingi unatoa nafasi kwa wanafunzi kukuza uwezo wa kusoma na kuandika pamoja na mbinu za kuweza kuhesabu (*basic literacy and numeracy*) na kuweza kuingiliana na mazingira yao. Wanafunzi wanajenga juu ya umilisi walioupata katika shule za chekechea na pia kuwaandaa kujiunga na shule ya msingi ya juu.

Mtaala unawasilisha Malengo ya Elimu ya Taifa, Matokeo yanayotarajiwa ya kiwango, kauli kiini, matokeo ya kijumla yanayotarajiwa, mada na mada ndogo. Mtaala pia unatoa matokeo maalum yanayotarajiwa, shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa, maswali dadisi yaliyopendekezwa, umilisi wa kimsingi, masuala mtambuko, maadili na pia viwango na vigezo vya kutathmini.

Ni matumaini yangu kwamba mitaala hii itatumiwa na mashirika ya serikali na washikadau wengine kupanga kikamilifu na kutekeleza wa Mtaala wa Kiumilisi.



**HON. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**
**WIZARA YA ELIMU**

## DIBAJI YA KATIBU MKUU

Mwaka wa 2019 Wizara ya Elimu ilizindua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kupitia mfumo wa ana kwa ana. Daraja ya chini ya Shule za Msingi ni kiwango cha kwanza katika elimu ya msingi baada ya masomo ya Chekechea katika muundo uliotolewa katika ***Basic Education Act of 2013*****. Mitaala iliyofanywa upya imejengwa katika msingi wa elimu ya Chekechea. Inawapatia wanafunzi nafasi ya kuingiliana na mazingira yao pamoja na kukuza mbinu za kusoma, kuandika pamoja na kuhesabu. Hii inaoana na ruwaza na mwito wa mageuzi ya mtaala kama inavyoelezwa katika** Mtaala wa Kiumilisi. Kiwango hiki cha elimu ni muhimu katika kuchangia kufikia ruwaza na mwito wa mabadiliko yanayoendelea ya kimtaala kama ilivyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Katika kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya. Mswada Elekezi huo unaeleza kuhusu kuvuka kutoka mtaala wa Kimafunzo na kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi

**Mitaala ya shule za msingi daraja ya chini katika juzuu tatu:**
**Juzuu ya kwanza: English Language Activities na Kiswahili Mazoezi ya Lugha.**
**Juzuu ya pili: Indigenous Language Activities na Creative Activities.**
**Juzuu ya tatu: Mathematical Activities, Environmental and Religious Activities.**

Mitaala hii inalenga kukuza umilisi wa mwanafunzi kwa kutoa maelezo yanayooana na mihimili ya Mtaala wa Kiumilisi. Mitaala hii pia inalenga kuelekeza wasomi kwa njia ifaayo na kusaidia ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi kufikia matokeo yanayotarajiwa. Inatoa mapendekezo ya shughuli za ujifunzaji za kimwingiliano ili kufanya ujifunzaji uwe wa kupendeza, kisisimua na kuburudisha.

**DKT. BELIO KIPSANG**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA AWALI NA E LIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

## SHUKRANI

Sheria Nambari 4 ya 2013 (Toleo jipya 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) inaipa uwezo Taasisi kukuza Mitaala na vifaa vya msaada kwa mtaala kwa elimu ya msingi na ya vyuo vya Elimu na Mafunzo. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote huhusisha utafiti, ulinganishi wa kimataifa, na uhusishaji mkubwa wa wadau wa elimu. Kupitia kwa mchakato huu wa utaratibu na wa kimashauriano, KICD ilizua wazo la Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (KICD), 2017. Unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Kanuni za Jumuia ya Afrika Mashariki na maelekezo kuhusu shirika la *International Bureau of Education.* *(*IBE) na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SGD).

KICD hufadhiliwa na Serikali ya Kenya ili kutekeleza majukumu na mipangilio ya serikali na sekta ya elimu. Pia, Taasisi hupata misaada kutoka kwa mashirika mengine ya kimaendeleo yanayoangazia miradi teule. Mitaala ya Gredi ya 1-3 imekuzwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Kenya Primary Education Equity in Learning Programme (KPEELP*), chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu. Tuna shukrani nyingi kwa msaada wa serikari kupitia Wizara ya Elimu na washirika wetu wa kimaendeleo kwa sababu ya sera, rasilimari na msaada pia wa kiufundi. Shukrani maalum kwa Waziri wa Wizara ya Elimu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Idara ya Serikali ya Elimu ya Awali na ya Msingi kwa mchango wao.

Ningependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wanaelimu wengine walioshiriki kama wanajopo, sekta mbalimbali za serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali walioshiriki kuandika mitaala hii ya Gredi ya 1-3. Kuhusiana na hili, ningependa kumshukuru Katibu wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC) kwa msaada wao katika mchakato wa kukuza mitaala hii. Mwisho, nalishukuru baraza la KICD kwa maongozi yake katika ukuzaji wa mitaala. Nawahakikishia waalimu, wazazi na washikadau wengine kuwa, mitaala hii itaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya 1-3 na kuwaandaa wanafunzi vilivyo kujiunga na Gredi za 4-6.

**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO, MBS**
**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU**
**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

## YALIYOMO

DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU .......... iii
DIBAJI YA KATIBU MKUU .......... iv
SHUKRANI .......... v
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA .......... vii
MGAO WA VIPINDI .......... ix
MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA YA ELIMU YA MSINGI .......... ix
KAULI KIINI .......... x
MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI .......... x
KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA GREDI YA 1 .......... 1
MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA .......... 84
KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA GREDI YA 2 .......... 90
MWONGOZO ULIOPENDEKEZWA WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA .......... 178
KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA GREDI YA 3 .......... 184
MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA .......... 268
KIAMBATISHO : SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL) .......... 274

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
   a) **Mahitaji ya kijamii**
      Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
      Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
      Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.
      Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
   Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira.**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

## MGAO WA VIPINDI

| | Somo | Vipindi Vilivyopendekezwa |
|---|---|---|
| 1. | Indigenous Language Activities | 2 |
| 2. | Kiswahili Language Activities / Kenya Sign Language Activities | 4 |
| 3. | English Language Activities | 5 |
| 4. | Mathematical Activities | 5 |
| 5. | Religious Education Activities | 3 |
| 6. | Environmental Activities | 4 |
| 7. | Creative Activities | 7 |
| 8. | Pastoral/Religious Instruction Programme | 1 |
| **Total** | | **31** |

## MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA YA ELIMU YA MSINGI

Kufikia mwisho wa elimu ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kuwasiliana apasavyo akitumia mbinu za mazungumzo na ishara katika miktadha mbalimbali,
b) kudhihirisha ufahamu wa hali ya juu wa dhana mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya kila siku,
c) kutumia ujuzi wa kijamii, mienendo na maadili ya kidini kwa nia ya kuchangia kukua kwa jamii,
d) kukuza talanta kwa nia ya kujiendeleza na kujifanikisha,
e) fanya maamuzi kutokana na ufahamu wa mambo kama mwananchi wa kitaifa na kimataifa mwenye jamii zenye demokrasia tofauti katika ulimwengu huru,
f) ibua mikakati bunifu inayoweza kuifadhi na kudumisha mazira,
g) kutumia ujuzi wa kidijitali kujifunza na kujifurahisha,
h) kufurahia haja ya umuhimu wa tamaduni nyingi na zenye utajiri kwa nia ya kutegemeana kwa binadamu.

## KAULI KIINI

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika shule za msingi. Somo hili humwezesha mwanafunzi kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Aidha, somo hili humwandaa mwanafunzi kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

## MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI

Kufikia mwisho wa kiwango cha chini, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano,
b) kuzingatia kanuni za lugha ili kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi,
c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali,
d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani,
e) kutumia hati za kimaandishi na mfumo wa kidijitali kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali,
f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

# KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA
# GREDI YA 3

## 1.0 UZALENDO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>c) kuthamini matumizi ya maamkuzi na maagano katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi na maagano *(k.v. Umeamkaje? Umeshindaje? Safiri salama, mchana mwema, usiku mwema)* kutoka kwenye chati, vitabu, kadi maneno, mti maneno, michoro, picha au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kujadili na wenzake picha, michoro, video n.k. zinazoonyesha vitendo vya maamkuzi na maagano,<br>● kuigiza maamkuzi na maagano akiwa na wenzake ili kujenga umilisi wa kutumia maneno haya,<br>● kujadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii yake. | Je, unajua maamkuzi na maagano yapi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuwasiliana na wenzake katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji.<br>● Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli mbalimbali za kikundi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposikiliza kwa makini maamkuzi na maagano mbalimbali kutoka kwenye vifaa vya kidijitali. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika mijadala ya maamkuzi na maagano darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>● Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya heshima na adabu katika maamkuzi na maagano. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapojadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii yake. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maamukuzi na maagano anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno 51- 54 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v. uzalendo, umoja, undugu, ushirikiano, upendo)* akiwa na wenzake,<br>• kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>• kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>• kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>• kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>• kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa ili amtolee maoni. | 1. Je, unapenda kusoma hadithi za aina gani?<br>2. Je, ni mambo gani unayoweza kujifunza kutokana na hadithi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi kutambua msamiati kuhusu suala lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili picha, kutabiri na kudhibitisha utabiri kuhusu hadithi. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotoa muhtasari wa hadithi aliyoisoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.<br>● Usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma ufahamu kuhusu suala lengwa na kuzingatia usalama mtandaoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Hati Nadhifu:** *Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3**) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu,<br>b) kuandika kifungu cha maneno kati ya 25-30 kwa hati nadhifu,<br>c) kufurahia kuandika kwa hati nadhifu ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mambo mbalimbali yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu *(k.v. muundo wa herufi, nafasi ifaayo kati ya maneno, nafasi zifaazo pambizoni, kutenganisha sentensi ifaavyo, usafi wa nakala)* kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu cha maneno yasiyozidi 30 kwa hati nadhifu kutoka kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 30 akizingatia hatua za uandishi *(k.v.* | Unazingatia mambo gani unapoandika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mambo ya kuzingatiwa ili kufanikisha hati nadhifu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli mbalimbali za kuandika.
- Ubunifu: mwanafunzi anaponakili kifungu cha maneno kwa hati nadhifu.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya maandishi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Matumizi ya Yeye na Wao**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua neno **yeye** na **wao** katika sentensi,<br>b) kutumia neno **yeye** na **wao** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kufurahia kutumia neno **yeye** na **wao** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaohusu **yeye** na **wao** kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua neno **yeye** na **wao** kutoka kifungu alichokisikiliza,<br>● kusoma vifungu na kutambua neno **yeye** na **wao** akiwa na wenzake au katika kikundi,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia **yeye** na **wao,**<br>● kutumia **yeye** na **wao** katika kuigiza mazungumzo na wenzake katika kikundi (k.v.*Yeye anasoma - wao wanasoma).* | Ni maneno gani unayoyatumia kuwataja wenzako bila kutumia majina yao halisi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutoa mifano kwa kutumia **yeye** na **wao**.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **yeye** na **wao**.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya **yeye** na **wao**.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia **yeye** na **wao** ifaavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi huku akisikiliza michango yao na kutoa maoni.

**Masuala mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maneno lengwa.
- Uraia: mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nafsi ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*

## 2.0 SHAMBANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Matamshi Bora:** *Vokali na Konsonanti za Kiswahili*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vokali za Kiswahili katika matini,<br>b) kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili katika matini,<br>c) kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>d) kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>**e)** kuchangamkia kutamka sauti | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vokali za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa,<br>● kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili,<br>● kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa,<br>● kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili,<br>● kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili (a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n, ng, ng’, ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z) zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kutambua vokali na konsonanti,<br>● kutambua vokali na konsonanti za Kiswahili katika kifungu kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutamka maneno, sentensi au kifungu chenye sauti za Kiswahili akiwa na wenzake, | Je, kwa nini ni muhimu kutambua sauti za lugha fulani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | za Kiswahili ili kuboresha matamshi. | ● kujirekodi akitamka sauti za Kiswahili akitumia vifaa vya kidijitali na kujitathmini pamoja au kutathminiwa na wenzake,<br>● kutamka sauti za kiswahili ipasavyo naye mzazi au mlezi ampe maoni yake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuzisikiliza, kuzitambua na kuzitamka vokali na konsonanti za Kiswahili.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili na kujirekodi akizitamka.
- Kujiamini: mwanafunzi anapozitamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwa mzazi au mlezi wake ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapokuwa makini kusikiliza vokali na konsonanti zikitamkwa na  mwalimu.

**Maadili:**

- Umoja:  mwanafunzi anaposhirikiana na wanzake katika shughuli za kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwenye kikundi kwa utulivu.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakiwemo walio na changamoto za kimaumbile.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali alivyotumia katika kujirekodi.

**Masuala Mtambuko:**

Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kuhusu suala lengwa.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /bw/, /fy/ na /kw/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa *(/bw/, /fy/, /kw/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 47 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*) akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k. akiwa na wenzake akizingatia | Je, utafanya mambo gani unaposoma ili uweze kusikika vizuri? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma kwa ufasaha akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa huku akizingatia matamshi bora, sauti inayosika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua sauti lengwa kwa ufasaha na kutumia vifaa vya kidijitali.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia kujifunzia.

**Masuala mtambuko:**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma hadithi yenye sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.
- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu na wenzake kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi kubwa katika matini,<br>b) kuandika kifungu cha hadithi akitumia herufi kubwa ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi kubwa katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua herufi kubwa katika kifungu kilicho kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kuandika kifungu chenye maneno **25-30** akizingatia maumbo ya herufi kubwa ifaavyo akizingatia hatua za uandishi (*maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa ili akitolee maoni. | Kwa nini tunatumia hati nadhifu katika uandishi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kuandika kifungu kwa kutumia herufi kubwa.

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi wake kifungu alichokiandika akitumia maumbo ya herufi kubwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika maumbo ya herufi kubwa ipasavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika kifungu.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kutathmini herufi kubwa alizoziandika.

**Masuala mtambuko:**

Masuala ya kijamii na kiuchumi: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia herufi kubwa ipasavyo.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika herufi kubwa anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>(**Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kutunga sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>• kusoma sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>• kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>• kuambatanishe umoja na wingi wa sentensi alizopewa kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali, n.k akiwa na wenzake,<br>• kuigiza michezo inayohusisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>• kutunga sentensi katika umoja na wingi wa sentensi akiwa na wenzake,<br>• kuwasiliana na mzazi au mlezi akitumia sentensi katika hali ya umoja na wingi ipasavyo. | Je, kwa nini unahitaji kutaja vitu katika hali ya umoja na wingi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika kuandika sentensi katika umoja na wingi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoeleza kuhusu vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi katika umoja na wingi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma sentensi katika hali ya umoja na wingi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza nyenzo zinazotumiwa katika ujifunzaji wa sentensi za umoja na wingi.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi akizingatia suala lengwa.
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine wanapotambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye matini.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nomino katika sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*

## 3.0 MIEZI YA MWAKA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Heshima na Adabu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu katika matini,<br>b) kutumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama michoro, picha au video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu akiwa na wenzake,<br>● kutambua maneno ya adabu na heshima kutoka kwa michoro, picha au video aliyotazama (tasfida) (*k.v. kwenda msalani*, *haja kubwa*, *haja ndogo*, *kuendesha),*<br>● kuigiza mazungumzo yanayoonyesha matumizi ya maneno ya heshima na adabu akishirikiana na wenzake,<br>● kujadiliana na mzazi au mlezi maneno ya heshima na adabu katika jamii yake. | Je, ni kwa nini tunatumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama picha, michoro na video kuhusu maneno heshima na adabu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua baadhi ya maneno ya adabu na heshima na matumizi yake. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu na heshima ipasavyo.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali ipasavyo.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika maigizo ya mazungumzo ya maneno ya adabu na heshima. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuigiza maneno ya heshima na adabu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya heshima na adabu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na miezi ya mwaka inayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 55 - 60 na kutambua msamiati wa suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kufafanua mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>● kumsomea mzazi au mlezi majina ya miezi ya mwaka aliyojifunza ili amtolee maoni. | Je, ni mambo yapi unaweza kujifunza kutokana na unachokisoma? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu katika kutabiri kitakachotokea katika hadithi.<br>• Uraia: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi kueleza ujumbe wa kifungu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma na kutoa utabiri katika kifungu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe katika kifungu.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anachotumia kujifunzia. Pia anapotekeleza majukumu aliyopewa anapofanya maigizo kuhusu miezi ya mwaka.<br>• Haki za kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijami: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka ukakamavu wake unajengeka. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na miezi ya mwaka inayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ipasavyo katika kifungu,<br>b) kuandika kifungu akitumia herufi ndogo ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi ndogo ifaavyo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ifaavyo katika kifungu kilicho kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>● kuandika kifungu chenye maneno 55-60 akizingatia maumbo ya herufi ndogo ifaavyo akizingatia hatua za uandishi *(maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>● kuwaonyesha wenzake kifungu alichoandika akizingatia maumbo ya herufi ndogo ili waitolee maoni. | Je, unazingatia mambo gani unapoandika herufi ndogo ifaavyo? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu jinsi ya kuendeleza herufi ndogo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kutumia kifaa cha kidijitali kutazama kielelezo cha uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,
- Kujiamini: mwanafunzi anapowaonyesha wenzake kazi aliyoandika ili waitolee maoni.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu mada lengwa kwa kutumia herufi ndogo.

**Masuala mtambuko:**

Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na miezi ya mwaka inayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Matumizi ya Maneno Yule na Wale**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **yule** na **wale** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya neno **yule** na **wale** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vyombo vya kidijitali nk. akiwa na wenzake,<br>● kusilikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya neno **yule** na **wale** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kujadili matumizi yake akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zilizotumia neno **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia neno **yule** na **wale** akiwa na wenzake,<br>● kuandika sentensi akitumia **yule** na **wale (***k.v Mtoto yule anacheza - watoto wale wanacheza)* na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili akamilishe sentensi akitumia **yule** na **wale,**<br>● kumsomea mzazi au mlezi kazi aliyoandika kuhusu matumizi ya **yule** na **wale.** | Unaweza kutunga sentensi zipi ukitumia maneno **yule** na **wale**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia maneno **yule** na **wale**.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya neno **yule** na **wale** akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia neno **yule** na **wale** kwa lugha fasaha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kwa kutumia neno **yule** na **wale**. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia neno **yeye** na **wao.**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

## 4.0 KAZI MBALIMBALI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Silabi za sauti /py/, /vy/ na /sh/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini,<br>d) kufurahia matamshi bora katika awasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/py/, /vy/, /sh/)* katika matini mbalimbali (*k.v kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali),*<br>● kutumia kifaa cha kidijitali *(k.v. kupitia programu ya papaya)* kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali (*k.v. kinasasauti na rununu)* akiwa na wenzake kisha azitamke, | Unazingatia mambo gani unapotamka maneno mbalimbali katika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakisomwa na mwalimu kisha atambue sauti lengwa katika maneno hayo,<br>• kutamka maneno yenye sauti ifaavyo akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kutoka kwa kitabu au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anashirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana katika kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshima matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika kutambua silabi za sauti lengwa.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kusoma kifungu chenye maneno ya sauti /*py/*, */vy/* na */sh/* kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma na kutunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matamshi bora anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4. 2.1 Kusoma kwa Ufasaha.** *Sauti /py/, /vy/, /sh/)* <br><br> **(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: <br> a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi, <br> b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora, <br> c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika, <br> d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo, <br> e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi | Mwanafunzi aelekezwe: <br> • kutambua sauti lengwa (*/py/, /vy/, /sh/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake, <br> • kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora, <br> • kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake, <br> • kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 49 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi*) akiwa na wenzake, <br> • kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake, | Je, unahakikishaje umesoma kifungu kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu.
- Uraia: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kusoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa.
- Kujithamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akitumia matamshi bora sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu cha maneno yenye sauti lengwa.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Nafasi ya Pambizo katika Uandishi**<br><br>**(Vipindi 3**) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya,<br>b) kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 60 akizingatia pambizo na aya,<br>c) kufurahia kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu na kutambua pambizo na aya kwenye kitabu, chati, kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali na kuwasomea wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake,<br>● kuandika na kumuonyesha mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ili ampe maoni yake. | Je, kwa nini tuzingatie nafasi za pambizo tunapoandika? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu akizingatia aya na pambizo.

| |
|---|
| ● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ipasavyo.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.<br>● Uzalendo: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia pambizo na aya.<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi na wenzake kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika kwa kuzingatia pambizo anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kuandika sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma sentensi katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kujaza nafasi kwa kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na mwenzake,<br>● kushiriki katika mchezo wa kusoma sentensi katika umoja na wingi na mwenzake,<br>● kuandika umoja na wingi wa sentensi akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizoandika katika umoja na wingi ili azitolee maoni. | Je, utajua vipi kama sentensi imeandikwa katika umoja au wingi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika sentensi katika umoja na wingi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapokamilisha sentensi katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi sentensi alizoandika katika umoja na wingi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi katika umoja na wingi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapoandika umoja na wingi wa sentensi.<br>● Haki za jamii: mwanafunzi aanaposhiriki katika mchezo wa kutunga sentensi kwa umoja na wingi na wenzake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi zinazohusiana na mapato ya watu na kazi mbalimbali. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana y umoja na wingi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

## 5.0 USALAMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaowasilishwa katika kifungu,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika kifungu alichosikiliza,<br>c) kutunga sentensi kwa kutumia msamiati uliotumika kwenye kifungu alichosikiliza,<br>d) kusimulia upya kifungu cha hadithi winalichokisikiliza,<br>e) kuchangamkia kusikiliza kifungu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kifungu cha maneno 60-65 kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali ili kutambua ujumbe unaowasilishwa,<br>● kutunga sentensi kwa kutumia msamiati aliousikiliza kwenye kifungu,<br>● kujibu maswali yanayohusiana na kifungu alichosikiliza,<br>● kujadili mambo muhimu katika kifungu alichokisikiliza akiwa na wenzake,<br>● kusimulia wenzake upya kifungu alichokisikiliza. | Je, unazingatia mambo gani ili kuelewa mambo unayoelezewa? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na kuwasiliana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za huduma kwa jamii kwa kusimulia visa vyepesi.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposimulia upya kifungu alichokisikiliza.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposimulia wenzake upya kifungu alichokisoma.

**Masuala mtambuko:**

Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposikiliza na kuzungumzia masuala ya usalama.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 60 - 65 na kutambua msamiati wa suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kufafanua mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu usalama wake shuleni. | Je, ni mambo gani unapaswa kuzingatia ili kufanikisha usomaji bora? |

- **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika kazi za kikundi wanapojadili ujumbe wa kifungu na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.

| |
|---|
| ● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma matini mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadiliana kuhusu ujumbe katika kifungu.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu na kutabiri.<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapowashirikisha wengine kufanya maigizo kuhusu usalama shuleni. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa jamii: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi na kutoa mchango wake, ukakamavu wake unajengeka.<br>● Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu masuala ya usalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Matumizi ya Kiulizi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya kiulizi katika maandishi,<br>b) kueleza matumizi ya alama ya kiulizi katika maandishi,<br>c) kuandika kifungu cha maneno kati ya 55-60 akitumia alama ya kiulizi ipasavyo,<br>d) kufurahia kutumia kiulizi katika maandishi ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua alama ya kiulizi kutoka kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kujadili na wenzake matumizi ya alama ya kiulizi ili kukuza uwezo wa kuitumia ipasavyo,<br>● kunakili ipasavyo kifungu kilichotumia alama ya kiulizi akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika kifungu cha maneno kati ya 55-60 akizingatia matumizi ya alama ya kiulizi kuhusu suala lengwa, na jinsi ya kuzingatia alama za usalama barabarani kisha kuwasomea wenzake ili waitolee maoni. | Je, alama ya kiulizi inatumika vipi katika uandishi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea kifungu alichoandika kwa kutumia alama kiulizi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu kwa kutumia alama ya kiulizi ipasavyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia alama ya kiulizi katika maandishi na pia anapotumia vifaa vya kidijitali. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoelekezwa kutangamana na mitandao ya kijamii kwa njia salama.<br>● Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika kifungu chepesi kuhusu suala la usalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya kiulizi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1. Matumizi ya -ake na ao.**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-ake** na **-ao** katika mawasiliano,<br>b) kutumia **-ake** na **-ao** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia -**ake** na **-ao** ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya -**ake** na –**ao** kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno au chati akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia –**ake** na –**ao** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa, au vifaa vya kidijitali,<br>● kusoma kifungu kilichotumia **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake,<br>● kuigiza matumizi ya **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake katika kikundi kwa kutumia vitu anavyomiliki (*k.v kiti chake – viti vyao),*<br>● kutunga sentensi akitumia -**ak**e na **-ao** na kuzijadili na mwenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **-ake** na**-ao,**<br>● kumtungia mzazi au mlezi sentensi zilizo na **-ake** na **-ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani. | Je, -**ake** na -**ao** hutumiwa vipi katika mawasiliano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi akitumia **-ake** na **-ao**.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutumia **-ake** na **–ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya**-ake** na **-ao**.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi kwa kutumia **-ake** na **-ao**. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu michango ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Masuala ya usalama: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia **-ake** na **-ao**. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

## 6.0 USAFI WA MAZINGIRA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*silabi za sauti /dh/, /th/ na /ch/*<br><br>(**Vipindi 3**) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifungu kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/dh/*, */th/* na */ch/*) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno, vifaa vya kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>● kuambatanisha silabi na kutamka maneno yanayotokana na sauti lengwa akiwa na wenzake, | 1. Je, matamshi bora hufanikisha vipi mawasiliano?<br>2. Je, ni mambo gani yanayozingatiwa ili kuboresha matamshi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa,<br>• kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa na kusikiliza na wenzake ili kuitathmini. | |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapoambatanisha silabi na kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. | | | | |

**Maadili:**

- Haki za jamii: mwanafunzi aposhirikiana na wenzake katika kutamka maneno ya silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kupotambua silabi za sauti lengwa.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi kinachohusu usafi wa mazingira akizingatia silabi za sauti lengwa na matamshi bora.
- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.

Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities*.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /dh/, /th/ na /ch/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (*/dh/, /th/ na /ch/*) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 51 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*),<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa | Je, utafanya nini ili kusikika vizuri unaposoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia katika kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi bila ubaguzi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu cha maneno kuhusu suala lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma hadithi kwa kutumia matamshi bora.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali kusoma hadithi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo *la English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Imla**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotamkwa kwenye imla ili kuyaandika ipasavyo,<br>b) kuandika kifungu cha maneno 55-60 yanayotamkwa kwenye imla akizingatia kanuni za uandishi zifaazo,<br>c) kuchangamkia kuandika kifungu akitumia maneno yanayotamkwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za uandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotamkwa yakizingatia suala na sauti */dh/*, */th/* na */ch/* na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali kutoka kwenye kitabu, chati, kapu la maneno n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini maneno yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali ili kuyaandika ipasavyo,<br>kuandika kifungu cha maneno 55-60 yatakayotamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali n.k. akizingatia kanuni zifaazo za uandishi,<br>● kujadili na wenzake kifungu alichokiandika ili kukitathmini,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia kanuni za uandishi zifaazo. | Unaposomewa chochote ili ukiandike, utafanya nini ili uandike ifaavyo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowaeleza wenzake maneno katika kifungu cha imla.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha imla akitumia kifaa cha kidijitali.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuandika maneno na kifungu cha imla.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika imla kwa kutumia maneno yenye sauti lengwa. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno 55-60 yatakayotamkwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabianchi: mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno yatakayotamkwa kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za maandishi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika imla anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo *la English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya -eupe, -eusi na -ekundu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yenye **-eupe, -eusi** na **-ekundu** ili kuyatumia ipasavyo katika mawasiliano,<br>b) kutumia**-eupe, -eusi, -ekundu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **-eupe, -eusi, -ekundu** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yenye **-eupe, - eusi, -ekundu** kwa kurejelea vitu halisi katika mazingira yake, kitabu, chati, vifaa vya kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maelezo kuhusu matumizi ya, **-eupe, -eusi, -ekundu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zinazotumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zenye matumizi ya **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga. | Je, vitu katika mazingira yako yana rangi gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia **-eupe**, **-eusi**, **-ekundu** akiwa na wenzake kutunga sentensi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza matumizi ya **-eupe**, **-eusi**,<br>• **ekundu**.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga akitumia **-eupe**, **-eusi**, **-ekundu**.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotumia maneno yenye **-eupe**, **-eusi**, **-ekundu** kutunga sentensi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotekeleza shughuli za darasani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

## 7.0 DUKANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi yanapotolewa darasani,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani,<br>c) kufurahia kuzingatia maagizo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua aina mbalimbali za maagizo kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake katika kutoa na kufuata maagizo mepesi kama vile (*k.v. simama uende uufungue mlango),*<br>● kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua aina mbalimbali za maagizo akiwa na wenzake,<br>● kuimba nyimbo na kukariri mashairi mepesi yanayohusu maagizo akiwa na wenzake,<br>● kumwimbia mzazi au mlezi wake wimbo unaoashiria maagizo ili atoe maoni yake. | Je,ni kwa nini mtu hufuata yale anayoambiwa? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika masimulizi na wenzake ya kufuata na kutofuata maagizo.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa maoni katika majadiliano kuhusu jinsi ya kufuata maagizo.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza maagizo mepesi akishirikiana na wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Amani: mwanafunzi anapofanya kazi katika kikundi na wenzake kwa utulivu.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapotazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwenye kifaa cha kidijitali bila usimamizi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu matumizi ya pesa dukani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo *la English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2. Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 65 - 70 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v duka, bidhaa, pesa, uza, nunua, chenji, mteja, muuzaji)* akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi akizingatia picha akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu kifungu baada ya kukisoma,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake. | Je, unazingatia mambo gani unaposoma kifungu cha hadithi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu wanapotabiri na kujadili ujumbe katika kifungu.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa na kuthibitisha utabiri wake kuhusu kitakachotokea katika hadithi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili picha na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.<br>• Haki za kijamii: mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika shughuli za kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotabiri kilichotokea katika kifungu alichokisoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu masuala yanayohusiana na shughuli za dukani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Uandishi wa Insha**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika kisa cha kati ya maneno 85-90 kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa kisa *(k.v. wahusika, ujumbe, muundo),*<br>● kusikiliza kisa kikitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>● kusoma kielelezo cha insha kwenye kitabu, chati au katika kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutambua kanuni muhimu za uandishi (*k.v. hati nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.*),<br>● kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na kujadili na wenzake; kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake,<br>● kumsomea kifungu kisha amwonyeshe mzazi au mlezi. | Je, ni mambo gani tunazingatia katika uandishi wa insha? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kujadili na wenzake kutambua vipengele vya uandishi wa insha.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika insha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na kujadili na wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake na kushirikiana katika shughuli za uhariri.<br>• Masuala ya kifedha: mwanafunzi anapoandika ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya uandishi wa insha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Ukanushaji wa nafsi ya tatu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi,<br>b) kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno, chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kutambua ukanushaji wa nafsi hiyo,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi,<br>● kutunga sentensi akitumia nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji wake (*kwa mfano: yeye anaandika - yeye haandiki),*<br>● kuigiza matumizi ya nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi sentensi za nafsi ya tatu umoja na wingi zilizokanushwa kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. | Unafikiri mwalimu wako alifanya nini jana? Iwapo hakufanya mambo uliyotaja ungesemaje? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji wake.<br>• Ujuzi wa kidijitali: wanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu katika shughuli za kikundi.<br>• Haki za jamii: mwanafunzi anapokanusha sentensi za nafsi ya tatu kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za ukanushaji.<br>• Masuala ya kifedha: mwanafunzi anapotumia ukanushaji katika sentensi zinazolenga masuala ya dukani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya uandishi wa insha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

## 8.0 NDEGE NIMPENDAYE

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Silabi za sauti /mbw, /nd/ na /ny/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa *(/mbw, /nd/, /ny/)* katika kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua silabi lengwa,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza yenye sauti lengwa; atamke na mwalimu na mwishowe atamke akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu cha hadithi na kutambua sauti lengwa, | Je, matamshi bora hukuzwa kwa njia gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kusoma kwa sauti kifungu kilicho na sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>● kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli mbalimbali ili kuboresha matamshi yake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na azisikilize na wenzake ili kutathmini matamshi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake, kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali katika shughuli inayorejelewa.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposoma kifungu kilicho na sauti *mbw*, *nd* na *ny* kuhusu suala lengwa kwa ufasaha na matamshi bora.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /mbw/, /nd/ na /ny/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa **(/***mbw***,** /*nd*/, /*ny*/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 53 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*),<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti | Je, ni kwa nini tunasoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo kwa ufasaha. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kwa ufasaha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma hadithi kwa ufasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu:  mwanafunzi anapojadiliana na wenzake na kusoma kifungu chepesi kwa ufasaha.

**Maadili**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.
- Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Tahajia**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi za maneno katika insha,<br>b) kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>c) kufurahia kutumia tahajia sahihi katika maandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua tahajia sahihi za maneno katika uandishi wa insha kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili kuhusu tahajia sahihi ya maneno katika kifungu kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno katika uandishi,<br>● kurekebisha insha akizingatia tahajia za maneno,<br>● kumsomea mzazi au mlezi insha aliyoiandika kwa kuzingatia tahajia za maneno. | Kwa nini ni muhimu kuendeleza maneno ipasavyo unapoandika chochote? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunza tahajia sahihi za maneno katika insha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji wa tahajia sahihi za maneno katika insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha kwa kuzingatia tahajia za maneno.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika insha akizingatia tahajia sahihi.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapojifunza kuandika insha kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi na tahajia sahihi.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika kuhusu tahajia anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4.Sarufi** | **8.4.1** Matumizi ya Maneno **Hili** na **Haya**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **hili** na **haya** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **hili** na **haya** katika kifungu ili kuboresha mawasiliano,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **hili** na **haya** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya neno **hili** na **haya** *(k.v. jicho hili – macho haya, jino hili – meno haya n.k.)* katika kifungu kwenye chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zinazoonyesha matumizi ya neno **hili** na **haya** katika kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia neno **hili** na **haya** akiwa na wenzake,<br>● kuandika kifungu kwa kutumia neno **hili** na **haya** na kujadili na wenzake ili kukitolea maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokitunga ili akitolee maoni. | Ni maneno yapi yanayoambatanishwa na maneno **hili** na **haya**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojenga msingi wa kujifunza zaidi kuhusu neno **hili** na **haya**.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia matumizi ya neno **hili** na **haya**.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotumia neno **hili** na **haya** kurejelea vitu katika mazingira yake. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia neno **hili** na **haya** ipasavyo<br>● Amani: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali na wenzake ili kutambua na kutunga sentensi akitumia **hili** na **haya** kwa utulivu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maneno lengwa.<br>● Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kutambua matumizi ya **hili** na **haya**. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vionyeshi na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

## 9.0 SOKONI

| Mada | Mada sNdogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala lengwa linalozungumziwa,<br>b) kuzingatia matamshi bora katika mazungumzo,<br>c) kujieleza kwa ufasaha kuhusu suala lengwa,<br>d) kutumia ishara zifaazo katika mazungumzo,<br>e) kuchangamkia mazungumzo katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua suala lengwa linalozungumziwa kupitia kwa picha kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali pamoja na wenzake,<br>● kuchukua muda wa kufikiri kuhusu suala la kuzungumzia,<br>● kupanga mawazo yake kuhusu suala lengwa na kuandaa hoja za kuzungumzia,<br>● kutamka maneno kwa kuzingatia matamshi yafaayo ya sauti mbalimbali,<br>● kueleza habari ambayo zinaleta maana na zenye kufuatana vizuri,<br>● kupandisha na kushusha sauti panapohitajika,<br>● kutumia ishara mbalimbali zinazohusiana na maelezo yake kuhusu suala lengwa, | Je, unazingatia nini unapozungumza kuhusu masuala mbalimbali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuzungumza na mzazi au mlezi wake akizingatia suala lengwa ili aimarishe mawasiliano. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza mazungumzo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo ya kila siku ili kuimarisha mawasiliano.
- Kujiamini: mwanafunzi anapojieleza kwa ufasaha mbele ya wenzake.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali na nyenzo nyinginezo anazotumia kujifunzia.
- Heshima: mwanafunzi anapowasikiliza wenzake darasani na kuheshimu maoni yao.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya mazungumzo na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities*.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2. Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 70- 75 na kutambua msamiati wa suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi kama akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa na kujadili ujumbe. | Je, ni mambo yapi unayozingatia unaposoma kifungu chochote? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofanya utabiri kutokana na picha.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma hadithi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake kushirikiana katika kusoma kifungu darasani.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa cha kidijitali darasani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya fedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha ya Masimulizi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia uandishi wa insha ya masimulizi ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza masimulizi yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali,<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya masimulizi kutoka kwenye masimulizi aliyosikiliza,<br>● kusoma kielelezo cha insha ya masimulizi kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali kuhusu insha ya masimulizi akiwa na wenzake,<br>● kutambua mambo muhimu katika uandishi wa insha katika kielelezo cha insha aliyosoma,<br>● kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa; kisa hiki kifuate hatua za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kisa kifupi kuhusu suala lengwa ili akitolee maoni. | 1. Je, unapenda kusimulia kuhusu nini?<br>2. Je,kisa ulichowahi kusimuliwa kilikuwa na mafunzo gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili vipengele vya uandishi wa insha.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu cha masimulizi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Uwazaji wa kina: mwanafunzi anapotambua mambo yanayotakikana katika uandishi wa insha ya masimulizi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia vipengele husika. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.<br>● Matumizi ya dawa za kulevya: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu matumizi ya dawa za kulevya zinazopatikana sokoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya uandishi wa insha na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1** Matumizi ya: ***Juu ya, Ndani ya na Mbele ya***<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu,<br>b) kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika matini,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kutoka kwa mgeni mwalikwa, mwalimu au vifaa vya kidijitali na kutambua matumizi yazo akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu kilichotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kujadili na mwenzake matumizi ya **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu ili kutolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kuigiza matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake kwa kutumia vitu anavyomiliki (*k.m*; *Mboga iko ndani ya gunia, Vitabu viko juu ya rafu, Kitabu kiko ndani ya mkoba, Gari liko mbele ya duka),* | Je, ni maneno yapi unayoweza kutumia kurejelea kitu/mtu aliye mahali fulani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kumtungia mzazi au mlezi wake sentensi kwa kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kwa kuzingatia vitu katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani y**a na **mbele ya.**
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo na vilevile anapofanya zoezi kwa kutumia tarakilishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowatungia wenzake sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya.**

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi huku akiyathamini maoni na michango ya wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi na pia anapotangamana na vifaa vya kidijitali.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kwa utulivu.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoigiza uuzaji na ununuzi akitumia **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya.**

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities*.

## 10.0 TEKNOLOJIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Sauti /mb/, /nz/ na /tw/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno na kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye silabi za sauti lengwa ili kufanikisha mawasiliano,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (/*mb*/, /*nz*/, /*tw*/) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa | Je, ni kwa nini tunatumia matamshi bora tunapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa akisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kifupi kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa kwa matamshi bora. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu chenye maneno ya sauti lengwa ili waitathmini na wenzake.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakisikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua silabi za sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /mb/, /nz/ na /tw/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (/*mb*/, /*nz*/, /*tw*/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 55 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*),<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi | Kwa nini ni muhimu kusoma kifungu kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo, sauti inayosikika na ishara zinazofaa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini usomaji wa wenzake darasani.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia.

**Masuala mtambuko:**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali inayohusu suala lengwa, awajibike na kuzingatia hatua za kiusalama.
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa pamoja na wenzake kutoka jamii mbalimbali.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kw ufasaha na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vinavyozingatiwa katika uandishi wa insha ya maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia kuandika insha ya maelezo ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo *(k.v wahusika, ujumbe, muundo)* kwenye kitabu, kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maelezo yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kielelezo cha insha ya maelezo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutambua kanuni za uandishi wa insha ya maelezo (*k.v. mwandiko nadhifu, mtiririko)* akiwa na wenzake,<br>● kuandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya maelezo na kuwasomea wenzake ili waitolee maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi insha ya maelezo aliyoandika. | Je, unatumia maneno ya aina gani unapotoa maelezo kuhusu kitu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposikiliza insha ya maelezo kutoka kwa kifaa cha kidijitali.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia vipengele vifaavyo. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa akizingatia hatua za uandishi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika insha ya maelezo na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vitendo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo katika matini,<br>b) kutumia vinyume vya vitendo ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vinyume vya vitendo (*k.v. fungua- funga, keti- simama, twika- tua)* kwenye chati, kitabu au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu chenye vinyume vya vitendo kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusoma vinyume vya vitendo katika kifungu akiwa na wenzake,<br>● kukamilisha sentensi akitumia vinyume vya vitendo akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake,<br>● kumtajia mzazi au mlezi vinyume vya maneno alivyojifunza darasani. | Je, unajua vinyume vipi vya vitendo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika vinyume vya vitendo katika sentensi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotekeleza shughuli ipasavyo.<br>● Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi pamoja na wenzake kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake kutoka jamii tofauti tofauti bila ubaguzi.<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua vinyume vya vitendo katika kifungu kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kuzingatia hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume vya maneno na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

**MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA**

**MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali Na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora.** **(***vokali za Kiswahili, konsonanti za Kiswahili;/py/,/vy/,/sh/, /mb/,/nz/,/tw/ /dh/,/th/,/ch/,/mbw/,/nd/ ,ny/*) | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa kikamilifu. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha.** *(kwa kutumia maneno ya heshima na adabu na mazungumzo ya kimuktadha)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno ya heshima na adabu na katika mazungumzo mbalimbali kwa uketo. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno ya heshima na adabu na katika mazungumzo mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia baadhi ya maneno ya heshima na adabu na katika baadhi ya mazungumzo. | Anazungumza na kujieleza kwa akitumia baadhi ya maneno ya heshima na adabu na katika baadhi ya mazungumzo kwa kuelekezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo.** **(***maamkuzi, maagano,kifungu na maagizo*) | Anasikiliza na kujibu maamkuzi, maagano na kifungu na kutoa na kufuata maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa urahisi. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi, maagano na kifungu na kutoa na kufuata maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi, maagano na kifungu, na kutoa na kufuata baadhi ya maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi maagano na kifungu, na kutoa na kufuata baadhi ya maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa kuelekezwa. |

**MADA: KUSOMA**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu – kifungu** *( ujumbe, matumizi ya msamiati mwafaka, kutabiri,kueleza mafunzo)* | Anasoma vifungu na kutambua ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo kwa utendeti. | Anasoma vifungu na kutambua ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo. | Anasoma vifungu na kutambua baadhi ya ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo. | Anasoma vifungu na kutambua baadhi ya ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo kwa kiasi. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma ufasaha kwa kuelekezwa. |

**MADA: KUANDIKA**

| Viwango<br>Vigezo | Kuzidi matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuandika kwa hati nzuri,** kutenganisha herufi ipasavyo na kuacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika kwa hati nadhifu unaosomeka, anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni kwa wepesi. | Anaandika kwa hati nadhifu unaosomeka, anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika kwa hati usio nadhifu lakini unaosomeka, anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika hati usiosomeka kwa urahisi, anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno na pambizoni kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha.** (*masimulizi, maelezo)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KuweKuweza kuzingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha.** | Anazingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha kwa utendeti. | Anazingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia baadhi ya alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia baadhi ya alama za uakifishaji na uendelezaji wa baadhi ya maneno katika uandishi wa insha. |

**MADA: SARUFI**

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia maneno mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. (***yeye, wao, huyo yule, wale, hili, haya, -ake, -ao, eupe, -eusi, -ekundu, juu ya, ndani ya, mbele ya)* | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya maneno katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya maneno katika matini kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno.** | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno kwa utendeti. | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno kwa kusaidiwa. |

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| *(Vinyume vya vitenzi)* | | | | |
| **Kuweza kutambua na kutumia umoja na wingi wa maneno, vifungu vya maneno na sentensi.** | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa maneno kwa utendeti. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa maneno. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa baadhi ya maneno maneno. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa baadhi ya maneno maneno kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi**.<br>*( ukanushaji wa nafsi ya tatu, vinyume vya vitenzi)* | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi kwa wepesi. | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi kwa kuongozwa. |

## KIAMBATISHO : SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL)

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya CSL ni kuambatanisha dhana zilizofunzwa darasani katika masomo mbalimbali na tajriba za maisha halisi ya mwanafunzi. Huwawezesha wanafunzi kuona jinsi mambo waliyojifunza yanavyohusiana na maisha ya kila siku. CSL huwa katika somo la *Environmental Activities*. Mwalimu darasani anatarajiwa kutambua na kuwaelekeza wanafunzi kutekeleza shughuli ya CSL ya darasa zima na jumuishi inayofaa kulingana na umri wa wanafunzi ndani ya shule. Usalama wa wanafunzi unafaa utiliwe maanani wakati wa kuchagua shughuli hii. Zifuatazo ni hatua za shughuli ya CSL jumuishi ambayo inafaa itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula wa shule.

| **Hatua za utekelezaji wa CSL jumuishi** |
|---|
| **1. Maandalizi**<br>• Amua shughuli itakayotekelezwa na wanafunzi.<br>• Tambua umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo mahususi kwa shughuli ya CSL.<br>• Tambua nyenzo hitajika kwa shughuli hiyo (vifaa vinavyopatikana karibu).<br>• Panga shughuli hiyo itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula (weka tarehe na saa ya shughuli).<br>• Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule, walimu na wadau wengine katika jamii ya shule.<br>• Tambua na ukuze vifaa vya kutathminia. |
| **2. Utekelezaji wa shughuli ya CSL**<br>• Wapatie wanafunzi majukumu.<br>• Hakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika shughuli hii.<br>• Watazame wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya CSL na uweke rekodi ya matokeo.<br>• Tumia kifaa kifaacho cha kutathmini mchakato wa shughuli na matokeo (tathmini kazi ya wanafunzi kutoka mwanzo hadi mwisho).<br>• Tathmini umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo. |

**3. Utafakuri wa shughuli ya CSL**

Kuwa na muda wa tathmini binafsi na wanafunzi kuhusu shughuli waliyotekeleza ya CSL jumuishi kwa kujadili yafuatayo:

- Ni nini kilifanyika vyema na kwa nini?
- Ni nini ambacho hakikufanyika vizuri na kwa nini?
- Ni nini kinachoweza kufanywa kwa njia tofauti wakati ujao?
- Ni nini wanafunzi walijifunza?

Kutakuwa na shughuli moja ya CSL kwa mwaka. Masuala makuu ya CSL jumuishi yatatokana na kategoria pana za masuala mtambuko na ujuzi unaolengwa katika masomo mbalimbali. Walimu wanatarajiwa kuwa na masuala tofautitofauti yanayolengwa kila mwaka ili kuwapa fursa wanafunzi kutalii masuala mtambuko mbalimbali. Kunafaa kuwa na uhusiano kati ya stadi za masomo na masuala makuu.

Shughuli ya CSL jumuishi itakuwa ya shule nzima ambapo jamii yote ya shule itahusika (wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika kupanga na kutekeleza shughuli ya CSL. Ingawa walimu huongoza upangaji na utekelezaji wa shughuli ya CSL, wanafunzi watatarajiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.

Shughuli hii ya CSL hutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatarajiwa kulenga umilisi na maadili tofautitofauti.

**Tathmini ya shughuli ya CSL**

Tathmini ya CSL jumuishi italenga vipengele 3 ambavyo ni: stadi kutokana na masomo mbalimbali yatakayojumuishwa katika shughuli hii, umilisi wa kimsingi uliokuzwa na maadili yaliyokuzwa. Tathmini inafaa kulenga mchakato mzima wa utekelezaji na matokeo ya mwisho ya shughuli. Mwalimu atatathmini wanafunzi katika vikundi akitumia vifaa mbalimbali kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, kiwango cha ukadiriaji na vifaa vingine faafu vya tathmini.